**Learning by Ear – Climate Change**

**Episode 08**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli:Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- MR KAPOOR – MD & OWNER NATIONAL POWER BOARD (60)
- MR WANGAI – BUSINESSMAN (50)

Scene 2:

- CAROL (14)
- JOSHUA (15)
- LORNA (16)
- MRS CHRISTINE KIMASI – RENEWABLE ENERGY INVESTOR (50)
- ALEX (15)

Scene 3:

- MRS KIMAU – SCIENCE TEACHER (45)
- GEORGE (15)

- LORNA (16)
- CAROL (14)
- JOSHUA (15)
- ALEX (15)
- ROBERT (16)
- HENRY (16)

**Intro:**

Karibu msikilizaji wa Deutsche Welle mahali popote ulipo kwa makala haya ya nane ya mchezo wa radio Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa. Maandaano yalifanikiwa. Na ni dhahiri kwamba wakaazi wengi wa eneo hilo wako tayari kuliunga mkono jopo kazi la wanafunzi katika kutafuta njia mbadala ya uzalishaji kawi inayozingatia usafi wa mazingira na inayoweza kutumika tena na tena katika kianda cha umeme cha Dhowville. Lakini katika makala haya, wanafunzi wanagundua kwamba hata kinyesi cha Ngombe pia kinachangia pakubwa mabadiliko ya hali ya hewa. Ungana nasi hadi mwisho ufahamu mengi zaidi.

**Scene One: Office of the National Power Board**

**SFX ATMO: OFFICE**

**1. MR KAPOOR**: Sasa unaona Bw. Mr Wangai, mambo hayaendi kama ilivyopangwa kuhusiana na mradi wa kiwanda hiki cha umeme. Mradi huu umechelewa kwa muda wa mwezi mmoja sasa..!

**2. MR WANGAI:** **(by conference call via phone)** Kwa hivyo unataka kusema ni wanafunzi wanne pekee waliopanga maandamano haya ya Dhowville, yaliyoangaziwa sana na vyombo vya habari?..... wanafunzi hao hao wanaopinga hadharani ujenzi wa kiwanda hiki?

**3. MR KAPOOR:** Ndio Bosi!. Wote hao wana njama ya kutushinikiza kutumia nishati isiyochafua mzingira na inayoweza kutumika tena na tena. Lakini ni vinyang´arika tu..!, na hawajui nini wanachotaka maishani au mahitaji ya mji huu. Unajua kisingizio chao ni kwamba kwamba kiwanda kitachafua mazingira,na pia kuchangia mabadiliko ya hali ya hewa, bla…bla …bla….Lazima pia sisi twende kwa vyombo vya habari kutoa taarifa ya kukanusha madai haya, na hata ikiwezekana kuwahonga waandishi wa habari. Na kisha labda tukutane na vijana hawa…..!

**(by conference call via phone)**

**5. MR WANGAI:** Kwa hivyo licha ya vitisho vyetu, unasema bado wamejitolea kufanikisha malengo yao?

**6. MR KAPOOR:** Ndio bwana Wangai.

**(by conference call via phone)**

**7. MR WANGAI:** Sawa basi nafikiri sasa ni wakati wa kutumia uwezo wetu kifedha kusukuma azma yetu. Wewe sasa utashughulikia suala la waandishi wa habari na kuandaa mkutano!

**SFX:** **CLICK AS LINE GOES DEAD**

## Scene Two: Cattle Farm

**SFX ATMO:** **COWS**

**8. CAROL:** Joshua, Kwa nini tunafanya mkutano huu katika zizi hili la ng´ombe?

| | |
|---|---|
| **9. JOSHUA:** | Errr, kusema kweli, Carol, sina uhakika…lakini huyu mwekezaji wa miradi ya kawi inayoweza kutumika tena na tena amepanga tukutane hapa. Nafikiri wanajuana na mkulima wa shamba hili la ng'ombe. |
| **10. CAROL:** | Ehhh , sawa basi! , ehh kuna mtu anakuja ! |
| **SFX:** | **CAR ARRIVING OPEN/CLOSE DOORS** |
| **11. MRS KIMASI**: | Habari Joshua. Nimefurahi kuwaona nyote hapa!. Habari…? mimi naitwa Christine Kimasi. |
| **12. CAROL:** | Jina langu ni Carol!. |
| **13. LORNA:** | Nami naitwa Lorna!. Sote tuna hamu kubwa ya kujua kwa nini tunakutana katika zizi hili la n'gombe! |
| **14. MRS KIMASI:** | Hata mimi nilijua tu mtakuwa na hamu ya kujua hayo.Lengo kubwa la kumleta hapa, ni kwamba najua mtakuwa na hamu kubwa kufahamu Ng'ombe hawa wazuru hivi pamoja na wengine wapatao bilioni 1.5 kote ulimwenguni huchangia kiasi cha asilimia 5 ya gesi inayochafua mazingira ulimwenguni.. |

| | |
|---|---|
| **15. ALEX:** | Wacha mzaha! |
| **16. CAROL:** | Nini? Eti ng’ombe pia wanachangia mabadiliko ya hali ya hewa?. Kivipi? |
| **17. MRS KIMASI:** | Wakati ng’ombe wanapoteuka hutoa gesi aina ya methani! |
| **18. JOSHUA:** | Sawa na ile gesi inayotoka kwenye majaa? |
| **19. MRS KIMASI:** | Hasa, Joshua. Ni hewa chafu inayotoka kwenye midomo ya ng’ombe hawa na wala sio ile ya kinyesi inayochafua mazingira.. |
| **20. JOSHUA:** | Lakini huwezi kuwazuia ng’ombe kuteuka!. |
| **21. MRS KIMASI:** | Kweli huwezi!. Lakini wanasayansi nchini Uingereza wamevumbua aina fulani ya chakula cha ng’ombe- yaani mchanganyiko wa majani makavu na nyasi ambao unatuliza tumbo la ng’ombe na kupunguza kiwango cha gesi inayoteukwa kwa asilimia 20. |

| | |
|---|---|
| **22. CAROL:** | Ni jambo la kushangaza!..., na kwa nini chakula hicho hakijafika hapa kwetu.? |
| **23. MRS KIMASI:** | Unajua inachukua muda mrefu kwa mambo kama haya au teknolojia mpya kufika katika mataifa yanayostawi |
| **24. ALEX:** | Sababu ni zile zile,- ukosefu wa fedha kuzuia mabadiliko ya hali ya hewa!. |
| **25. MRS KIMASI:** | Unakosea Alex. Tunaweza kuchangisha pesa kufadhili miradi hii endapo tutawasilisha mapendekezo mazuri na kuwashawishi watu wengi kutuunga mkono.. |
| **26. LORNA:** | Kwa hivyo bibi Kimasi, nini mawazo yako kuhisiana na kiwanda hiki cha umeme. Je una mipango yoyote? |
| **27. MRS KIMASI:** | Kusema kweli, kwa kuzingatia eneo kitakakojengwa kiwanda hiki, na rasilimali zilizopo katika mji huu wa Dhowvile, nadhani zipo njia kama 3 hivi mbadala za kuzalisha nishati isiyochafua mazingira.. |

| | |
|---|---|
| **28. CAROL:** | Eti tatu? Zipi hizo? |
| **29. MRS KIMAI:** | Nadhani, Carol, tunaweza kutumia nishati inayotokana na mimea, upepo na maji. |
| **30. CAROL:** | Kawi inayotokana na mimea? |
| **31. MRS KIMASI:** | Ndiyo, inategemea mahali inakozalishwa. Gesi inayotokana na mimea inajulikama kama gesi ya ***kinamasi.***. Kwa ufupi ni gesi inayotokana na vitu vilivyooza kwenye jaa, ambayo hunaswa na kisha kutumiwa kama kawi. |
| **32. LORNA:** | Sasa inapatikana tu kwenye kwenye majaa? |
| **33. MRS KIMSAI:** | Hapana pia unaweza kuzalisha au kupata aina hii ya gesi kutoka kwa mbolea, mabomba ya maji taka katika sehemu za miji au hata mimea na kinyesi cha ng'ombe.. |
| **34. LORNA:** | Lakini kwa ufupi tunaweza kutumia majaa kutengeneza aina hii ya kawi? |

**35. MRS KIMASI:** Ndio, hiyo inawezekana!

**36. ALEX:** Pia ulisema kinyesi cha ng’ombe?

**37. MRS KIMASI:** Ndio. Nchini India watu binafsi hutumia kinyesi cha ng’ ombe wanaowafuga kutengeneza gesi ya kupikia.

**38. CAROL:** Ni jambo la kushangaza sana! Kwa hivyo ingawa ng’ombe hawa wanateuaka gesi chafu inayoathiri mazingira, kwa upande mwengine wana manufaa makubwa!

**39. MRS KIMASI:** Kabisa, sasa tuachane na ng’ombe, na tuondoke hapa, maana sasa harufu ya uvundo wa kinyesi imezidi –Twendeni mjini tujadiliane njia nyingine zilizosalia?

**40. JOSHUA:** Sawa, twendeni!

**Scene Three:**

**SFX ATMO:** **CLASSROOM**

**41. MRS KIMAU:** Nyamazeni! Bado tunajadili suala la mabadiliko ya hali ya hewa. Jukumu lenu sasa ni kupitia magazeti yote na pia mtandaoni kutafuta mifano ya hivi punde kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa kote ulimwenguni. Nani ataanza?

**42. GEORGE:** Mimi nimesoma kwamba rais mpya wa kisiwa cha Maldives – tajiri mkubwa katika kisiwa hicho ameanza kuwatafutia makao watu wake kwa sababu kisiwa hicho kimeanza kuzama kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa!

**43. MRS KIMAU:** Huo ni mfano mzuri sana, George. Unaweza kutufahamisha zaidi?

**44. GEORGE:** Kuna zaidi ya visiwa 1,200 na asilimia 8 ya visiwa hivyo vimezama na kusalia mita moja tu juu ya bahari. Sawa na urefu wa dawati! Wataalam wanasema kuwa katika muda wa muongo mmoja ujao, visiwa hivi havitakuwepo tena!

**45. CAROL:** Kwa hivyo kina cha bahari kinaongezeka kila mwaka?

**46. GEORGE:** Ndiyo, hivyo ndivyo nilivyosoma! Baadhi ya wakaazi sasa wameanza kuhama kisiwa kimoja kutokana na mafuriko ya kila baada ya wiki mbili kufuatia ongezeko la mawimbi baharini.

**47. CAROL:** Na kuongezeka huko kwa kina cha bahari kunatokana na mabadiliko ya hali ya hewa pia?

**48. MRS KIMAU:** Ndiyo Carol. Kadri kiwango cha joto kinavyozidi kuongezeka duniani, joto zaidi linaelekezwa baharini. Na kama mjuavyo, wakati vitu vinapopata joto, hupanuka. Kwa hivyo kupanda kwa kiwango cha joto ulimwenguni husababisha kuongezeka kwa joto baharini.

| | |
|---|---|
| **49. GEORGE:** | Na kwa hivyo kadri inavyozidi kuwa joto ardhini ndivyo kiwango cha joto baharini kinavyozidi kuongezeka na kuyeyusha barafu katika maeneo ya baridi kali. Na ndio sababu barafu inaendelea kuyeyuka katika maeneo ya milima. Hali hii huongeza kiwango cha maji baharini na hivyo kuongeza kina hicho. Oh na pia nimesoma kwamba katika visiwa hivyo vya Maldives, hali ya hewa imebadilika kwamba wavuvi sasa hawawezi tena kubashiri misimu ya mvua, kama ilivyo hapa kwetu. |
| **50. MRS KIMAU:** | Ni jambo la kushangaza, George. Na tayari nchi nyingine zimeanza kushuhudia mparaganyiko wa misimu ya mvua kama tunavyoshuhudia hapa. |
| **51. GEORGE:** | Oh, na pia bi Kamau, nimesoma kwamba visiwa hivyo vya Maldives vilikuwa mstari wa mbele kutia saini mkataba wa kuhifadhi mazingira wa Kyoto. |
| **52. MRS KIMAU:** | Unaweza kutueleza zaidi kuhusu mkataba huu wa Kyoto George? |

| | |
|---|---|
| **53. GEORGE:** | Ni mkataba uliofikiwa baina ya mataifa mbali mbali katika juhudi za kupunguza utoaji wa kiwango cha gesi na moshi unaochafua mazingira hewani, ili kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa? |
| **54. MRS KIMAU:** | Ndio lakini ni mataifa mengi yaliyotia saini mkataba huu! Na miongoni mwayo ni mataifa yenye uwezo mkubwa kiviwanda yanayotoa kiasi kikubwa cha moshi na gesi inayochafua mazingira. |
| **57. GEORGE:** | Lakini tatizo ni kwamba bara la Afrika ndilo linaloathirika zaidi na mabadiliko haya ya hali ya hewa licha ya kwamba bara hili halitoi kiasi kikubwa cha gesi inayochafua mazingira ikilinganishwa na mataifa yaliyostawi. |
| **SFX:** | **BELL** |
| **59. MRS KIMAU:** | Sawa, kengele sasa imelea, tutaendelea na mjadala wetu na kupata mifano zaidi katika somo letu lijalo. |
| **SFX:** | **SCRAPING CHAIRS/CHATTER** |

| | |
|---|---|
| **60. HENRY:** | Habari Lorna, nadhani sasa mtatupilia mbali mpango wenu wa kuendelea kupinga ujenzi wa kiwanda cha umeme. |
| **61. ROBERT:** | Ndio, hata, mamangu anasema hivyo pia. Anasema kuwa habari zilizotangazwa redioni ni kwamba nyinyi wanafunzi wanne mnatatiza juhudi za kupatikana kwa umeme na maendeleo ya mji huu wa Dhowville! |
| **62. LORNA:** | **(fighting)** Robert, hebu niache na mambo yangu!. Usinisukume! Una maana gani kusema umesikia kwenye radio? |
| **63. HENRY:** | Nenda usome gazeti la leo! Kila mmoja anasema kuwa nyinyi ndio wakulaumiwa endapo umeme hautapatikana hapa. |
| **64. ALEX:** | **(running up)** Wewe… wewe , Henry, muache! Usimusukume namna hiyo huyo msichana! |

| | |
|---|---|
| **65. ROBERT:** | Hata wewe Alex! Wakaazi wa mji huu hawatakubali vinyang´arika kama nyinyi mtukoseshe umeme hapa! |
| **SFX:** | **SLAMMING OF DOOR** |
| **66. JOSHUA:** | Lorna, Kunaendelea nini hapa? Nimemuona Robert akikusukuma. |
| **67. LORNA:** | Ndio Joshua. Inaonekana wale wazee wa bodi ya kiwanda cha umeme wameanza tena kutumia mbinu zao kututisha kama kawaida. Bila shaka wamewahonga waandishi wa habari ili kukandamiza juhudi zetu. |
| **68. CAROL:** | Siamini kwamba wanafunzi wenzetu pia wametugeuka. Nadhani sasa wakati umewadia kutafuta usaidizi kutoka kwa waziri wa mazingira bwana Gitaki. Alisema anaweza kutusaidia! Hebu twendeni! |

## END OF EPISODE 8

**Outro:**

Na hadi hapo tunafika mwishi wa makala haya ya Noa Bongo Jenga Maisha yako kwa leo. Usikose kuungana nasi wakati mwengine wakati jopo la wanafunzi hawa litakapokutanna na wakereketwa wa wa ujenzi wa kiwanda hiki. Mchezo huu kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa umeandikwa na Victoria Averill. Pia ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtandao wetu wa DW-WORLD.DE/lbe. Hadi wakati huo basi kwaheri kwa sasa na Asante kwa kusikiliza!